**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Mwaka……………….**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MKINDI,**

**S.L.P. 90,**

**KILINDI - TANGA.**

**TAREHE …………….**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................................................................**

**S.L.P ...........................…………………………………**

**Yah: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MKINDI HALMASHAURI YA KILINDI ILIYOKO MKOA TANGA MWAKA ……</u>**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule yetu kwa mwaka ……. na atasoma tahasusi ya HGK,HGFa,HGL na HKL Shule ya Sekondari Mkindi ipo mkoa wa Tanga umbali wa Kilometa 28, kutoka Mji wa Handeni Usafiri wa basi kutoka mjini Handeni unapatikana katika kituo cha mabasi Handeni Nauli ni Shilingi 3000 shuka Msente na chukua pikipiki sh 5000 mpaka shuleni, na ukishuka Handeni waweza kuja kwa pikipiki moja kwa moja mpaka shuleni kwa Shilingi 10,000/= kwa bajaji 20000/= .

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 SARE ZA DARASANI**

i. Sare ya shule hii kwa wasichana ni mshono wa sketi ni V mbele isiyobana na ndefu mpaka chini.
ii. wavulana suruali sio modo (kitambaa ni lucas *rangi ya bluu sio dark bluu kwa wote jozi2*). Unaweza kushona mwenyewe au kuja kushonea karibu na shule kwa gharama ya 25000/= kwa moja hii ni kuepuka kuchanganya rangi.
iii. Mashati mawili mawili meupe ya mikono mirefu anakuja nayo.

iv. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
v. Aje na T-shirt ya darasani rangi ya khaki atakaye kosa T-shirt hiyo yenye nembo ya shule **endapo utakosa** inapatikana shuleni kwa sh 13000/= kwa wote. Itavaliwa siku ya jumatano na ijumaa darasani.
vi. Tai 1 ya bluu ya kati yenye michirizi meupe zinapatikana madukani.
Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.
vii. Sweta rangi ya kijivu yenye mshono wa V shingoni.
viii. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
ix. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi au juma na roza kwa wasichana.

**NB.** Watoto wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele au kupaka rangi kucha.

### 1.2 SARE ZA KUSHINDIA NA MICHEZO

i. Nguo za kushindia gauni 1 rangi ya kijivu isiyoiva mshono wa dera refu mpaka chini na sketi 1 ya kijivu isiyo iva mshino wa solo kwa wasichana kitambaa kizito. xi. Suruali isiyo bana rangi ya kijivu isiyo iva kitambaa kizito kwa wavulana.
ii. Aje na T-shirt za kushindia rangi ya blue bahari atakaye kosa, zenye maandishi ya shule zinapatikana duka la karibu na shule kwa sh 13,000/=.
iii. Sare ya Michezo ni track suit za nyeusi yenye nembo au mistari ya bendera ya Tanzania pembeni kwa wote
iv. Aje na jezi ya Tanzania (Taifa stars) yenye mistari ya njano na bluu.
v. Raba za michezo kwa wote au viatu vya mpira (njumu).

**NB.** Kila mwanafunzi aandike jina Lake kwenye sare zake na vifaa vyake.

### 1.3 MAHITAJI YA DARASANI

i. Madaftari 8 counter book quire 3,na madogo 7 ya mazoezi
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Scientific Calculator.
v. History -History for secondary school form 5&6 by TIE
vi. Essential History for secondary school paper1&2 by SalehYasin
vii. Kiswahili -Sarufi kidato cha 5&6 cha TIE
viii. Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5&6 cha Nyambali Nyangwine au TIE
ix. Geography- A Comprehensive Approach to physical Geography by DT Msabila
x. Practical Geography; map reading photography Advance level 5&6
xi. Kamusi ya kiswahili sanifu nk.

### 1.3 MAHITAJI YA BWENINI NA VIFAA VYA USAFI

xii. Godoro futi 2 na nusu.

xiii. Mashuka Jozi 2 moja nyeupe na moja pink kwa wasichana,na shuka 2 za bluu kwa wavulana ,blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1cheupe wasichana na dark bluu wavulana .

xiv. Nguo za ndani za kutosha;na singlend nyeupe na blazia nyeupe xv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xvi. Panga 1 Brashi za kusugulia sink mifagio 1 wa chelewa wenye mpini wa mti kwa wote Soft bloom na reki kwa wasichana

xvii. Rubber squizer na jembe kwa wavulana.

xviii. Aje na bima ya afya.

xix. Aje na tochi ya betri au taa ya sola kwa tahadhari umeme ukikatika.

### 1.5 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Ilipwe kwenyewe namba ya akaunti **NMB 42610000565** jina Mkindi Secondary School na aje na benk slip

## 2 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na.

**1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kufuga nywele au kusuka. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ii. Uvutaji wa sigara;
iii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
iv. Kusababisha mimba;
v. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
vi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
vii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
viii. Kudharau Bendera ya Taifa au wimbo wa taifa.
ix. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
x. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**NB;**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Kama hujaelewa tafadhali piga simu kwa Namba zilizopo.

**PRIME MINISTER'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT MKINDI HIGH SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS**

MKINDI SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 90,
**SONGE – KILINDI**

Date.......................

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMENT HOSPITAL**

NAME OF STUDENT.........................................................................................
Please examine the above named student to ascertain his fitness for admission to pursue studies.

................................................
**Head Mistress/Headmaster**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin.......................................................................................................................
Eyes.......................................................................................................................
Ears.......................................................................................................................
Chest.....................................................................................................................
Spleen...................................................................................................................
Abdomen...............................................................................................................
Urine.....................................................................................................................
Stool.....................................................................................................................
Hemoglobin (Hb)..........................................................................................
I consider that:

- He is of good health, free from infectious diseases, worms, bilharzias and fit to pursue studies
- He is now fit to return to school after having been treated for................

..................................................**Name and Designation** **Signature**

**…………………………..** **……………………….**
**Official Stamp Date**

## UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MKINDI

**SEHEMU A:** (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi (jina kamili)...............................................................................

Tarehe ya kuzaliwa..................................................................................

Dini........................................................................................................

Kijiji............................. Wilaya............................... Mkoa.........................

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidatocha Tano Shule ya Sekondari Mkindi. Nathibitisha kuwa Nitatii na kufuata sheria zote za Shule kama zilivyo ainishwa. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika Migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini.............................................          Tarehe..........................................

**SEHEMU B:** (Ijazwe na Mzazi)

Mimi (Jina kamili) ................................................Namba ya

simu........................ Kijiji..................................

Wilaya............................. Mkoa...............................

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mwanangu Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya Shule. Nitahakikisha mtoto anaenda shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi..........................................Tarehe....................................... Jina la

Mtendaji wa Kijiji...............................................................................

Saini................................ Tarehe............................ Mhuri.........................

Jina la Mtendaji Kata..................................................................................

Saini................................ Tarehe............................Mhuri………………………

**PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU WATAKAOWASILIANA AU KUFIKA KUMTEMBELEA AWAPO SHULENI**

1. Picha

Jina(Matatu)

______________________________________

Uhusiano na mwanafunzi ______________________

Namba za simu ___________________________

2.Picha

Jina (matatu)

______________________________________

Uhusiano na mwanafunzi ____________

Namba za simu ___________________

3. Picha

Jina(matatu)

______________________________________

Uhusiano ____________________

Namba za simu __________________________

4. Picha

Jina(matatu)

______________________________________

Uhusiano ________________

Namba za simu _______________

**NB: Hatarusiwa mtu mwingine yoyote kumtembelea au kufanya nae mawasiliano akiwa hapa shuleni. Siku ya kuwatembelea wanafunzi ni kila wikendi ya mwisho wa mwezi.**

**ANGALIZO**

Hakikisha unafika Shuleni ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule na mwisho wa kuripoti ni wiki mbili kuanzia tarehe ya kufungua Shule na baada ya hapo nafasi yako atapewa mtu mwingine endapo utakuwa hujafika Shuleni.

KARIBUNI SANA MKINDI SEKONDARI

**.......................................**

**LAWI J. MTALIMILE**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0773 957782/ 0627372743**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0711949748/0710224333**
- **Mwandamizi Taaluma 0659807445**
- **Mwandamizi Malezi 0714 569192/ 0657586767**